**Dondoo za mkutano wa Umma wa Wapanda Baiskeli Dar es Salaam**
**Tarehe 1 Septemba 2007**

**Waliohudhuria**
Ally Saidi Mohamedi
Dominata Rwechunguiza
Elaine Baker
Filbert Mbecha
Frank Peter Rioeyongeza
Juma Ali Salehe Jongo
Juma Imori Rugole
Jumanne Idd Selemani
Patrick Masinga
Patrick Maziku
Paulo Atibu Hatibu
Rahma Ali
Sosthenes C Amlima
Sudi Saidi Ramadhan

**Wageni**
Godfrey Jax – CHABADA
Hussein Ally - CHABADA

**Msafara wa Baiskeli**
Ilipangwa hapo awali kuwa leo tutakuwa na kikao cha kamati ndogo ya msafaro wa Baiskeli kwa muda na mahali kama ilivyochaguliwa na AALOCOM, lakini hawakusema kitu tulipo wapigia simu na hivyo basi CHABADA walihudhuria kikao cha UWABA. Bw. Mlamba wa AALOCOM alisema kwamba Bw. Majembele atakuja kwenye kikao cha UWABA, lakini hakuja. Jax alisema kwa kuwa hakukuwa na watu wengi wa kamati ya Msafara ili kuchagua viongozi, jambo hili lifanyike badae (siku nyingine). Jax alisema atatembelea ofisi za AALOCOM Jumanne kuuliza kama kweli wanataka kuwa sehemu ya maandalizi ya msafara au la.

Elaine alisema alimpigia simu Mh. Azzan Zungu Mbunge kufuatilia ahadi aliyoitoa kuhusu msafara. Alishauri tuandike barua kwa Meya wa Manispaa ya Ilala kuomba kutumia Mnazi Mmoja bila malipo, lakini tuipeleka barua hiyo ofisini kwake ili afuatilie yeye mwenyewe kwa meya. Juma alipeleka barua hiyo Alhamisi na Azzan Zungu aliahidi kufuatilia .

Ilijadiliwa kuwa tunahitaji kivuli ili washiriki wasikimbilie vivuli vya miti ambavyo vitakuwa mbali na jukwaa Mnazi Mmoja, kama ilivyokuwa mwaka jana. Ilikubalika kumuomba Mh. Azzan Zungu kuhusu kuruhusu kutumia vivuli vya maturubai katika viwanja vya Mnazi Mmoja.

Jumatatu Paulo alipeleka barua kwa Bakhresa na Kampuni ya Guta kuwashukuru kwa kutoa maji na guta na kuwakaribisha kushiriki katika msafara.

Siku ya jumatatu Elaine na Paulo walikwenda ubalozi wa china. Tuliowakuta huko walikuwa na msaada sana na walitupa namba ya simu ya katibu wa Balozi, ambae hakuwepo ofisini wakati ule. Alisema Balozi alikuwa kamaliza muda wake na Balozi mpya alikuwa anakuja hivyo tufuatilie baada ya ujio wa balozi huyo mpya.

Elaine na Paulo pia walipeleka barua ya kuomba ufadhili kwa Bw. Mengi IPP siku ya jumatatu.

Celtel (Bibi Tuno) alisema bado wanafuatilia barua yetu ya kuomba ufadhili. Katika ubalozi wa Uholanzi, Harriet Samson alikuwa kwenye vikao mara nyingi, Elaine alimpigia simu wiki hii. Knight Support waliendelea kutuambia tuwapigie simu tena baada ya siku kadhaa mara kwa mara, Elaine huwapigia.
Ilikubalika kuwa Juma na Elaine watatembelea Knight Support na Celtel jumatatu kufuatilia na wataendelea kupiga simu kwa wengine.

Jax alisema atomba DSI ambayo husambaza vifaa (Vipuri) vya baiskeli kuchangia magurudumu na kofia kama zawadi za bahati nasibu.

Ilijadiliwa kuhusu kuandaa mabango mengi zaidi kuongezaea yale yaliyotumika mwaka jana. Sosthenes aliseama kwamba vifaa vya kutengeneza mabango 15 vitagharimu karibu Tsh. 35,000/= alitoa Tsh. 7000/= za guta kwa wiki hiii na Elaine na Juma watachukua Tshs. 28000 kutoka benki jumatatu ili Sosthenes atengeneze mabango. Ilikubalika kutumia kauli mbiu ile ile ya mwaka jana.

Kulitangaza tukio hili pia kulijadiliwa. Dominata alisema kwamba ana mawasiliano mazuri na vyombo vingi vya habari kupitia watu wanaofanya kazi humo na hivyo basi ilipendekezwa kuwa na tangazo rasmi kuhusu msafara ambao pia atawaalika. Ilikubalika kwamba Elaine na Dominata watatoa matangazo na Dominata atawakaribisha wanahabari katika kikao siku ya jumamosi wiki ijayo kwa ajili ya matangazo saa 5 asubuhi. Elaine alisema atawatumia ujumbe wajumbe wote wa UWABA kuwa taarifu na Jax atawataarifu wanachama wa CHABADA.

Ilijadiliwa kwamba tunahitaji kipaza sauti na muziki. Hussein Ali alisema ana vifaa hivyo na yuko tayari kuvitoa kwa ajili yetu bure, lakini kwa sasa ni vibovu vinahitaji marekebisho. Atatupa taarifa wiki ijayo kama marekebisho yamemalizika.

Ilikubalika kutumia barua maalumu za mwaliko kwenye msafara kwa SUMATRA, Chuo cha Taifa cha Usafirishaj, askari wa usalama barabarani, waziri wa miundombinu, Mameya wa Temeke, Kinondoni na Jiji la Dar es Salaam (Meya wa Ilala tayari alikuwa amealikwa), TANROADS, HUWATA na chama cha walemavu Tanzania (CHAMWATA) Buguruni.

Ilikubalika kutengeneza vipeperushi na mabango sawa nay a mwaka jana.

**Ofisi**
Juma ameongeza taarifa / maelezo zaidi kwenye ubao wa matangazo ilijadiliwa kwamba ubao wa matangazo uwe na sehemu tofauti za dhamira kuliko kuchanganya zote. Ally Saidi Mohammedi alisema kwamba hakuwa na nafasi ya kutengeneza shelfu na kutengeneza fremu na meza wiki iliyopita ili atafanya hivyo wiki ijayo.

**Guta**
Jumanne ameleta Tsh 7,000 kama mwendelezo wa wiki ya kwanza ya matumizi ya guta na kumpa Juma ambaye alimpa Sosthenes ili kutengeneza mabango.

**TANROADS**
Jumatatu Elaine na Paulo aliwapigia TANROADS nakuongea na mhandisi aitwaye Massawe ambaye ni Mkurugenzi wa miradi. Alisema alikuwa anaandika barua kujibu barua yetu kuhusu barabara tatu zilizo ujenzi na ingekuwa tayari baada ya siku chache. Tuliomba kufanya mkutano ambapo tutatoa mada kuhusu barabara za Dar es Salaam.

**Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam**
Ilitambuliwa kwamba halmashauri ya jiji haijajibu barua yetu kuhusu mpango madhubuti wa usafirishaji Dar es Salaam au kutualika (kama walivyoahidi) kutoa maelezo kuhusu ubunifu wa barabara ya Morogoro kwa mradi wa DART ilikubalika kwamba Paulo atafuatilia wiki hii na kuwapeleka nakala ya barua na kutaka majibu.

**Mradi wa Usalama wa baiskeli/ wamba Memorial Fund.**
Elaine alisema amepata barua pepe kutoka kwa profesa Osili wa wamba Memorial Fund kuthibitisha kupata pendekezo tulilotuma na kwamba watatujulisha kuhusu matokeo mwezi octoba.

**Vitambulisho**
Elaine alionyesha vitambulisho vilivyobuniwa vikiwa na alama ya guta, baiskeli ya walemavu na anuani yetu na mahali ili wanachama watie sahihi. Ilikubalika kwamba wanachama watie sahihi kwenye vitambulisho kwenye mkutano na Paulo atavikamilishia magomeni. Juma, Jumanne Rahma, Paulo, Filbert, Maziku , Sudi Saidi na Patric masinga waliomba vitambulisho vipya vyenye ubunifu mpya.

**Mhuri**
Wakati wa wiki Paulo alileta mhuri uliotenenezwa na wino kwa mchango kutoka kwa Elaine. Huu utatumika kwenye barua zetu.

**T-shirt**
Sosthenes alikubali kutafuta gharama za kuchapisha  t-shirt